KUMBUKUMBU
ZA
MKUTANO WA DUA

Na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi

ISLAM INTERNATIONAL PUBLICATIONS LTD

Kumbukumbu za Mkutano wa Dua

Tafsiri ya Kiswahili ya: Ru’idaad-e-Jalsa-e-Du‘aa (Kiurdu)

Proceedings of the Prayer meeting (Swahili Translation)

Mwandishi:
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Qadian

Mfasiri:
Sheikh Khurram Shahzad

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1900
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2025

© Islam International Publications Ltd.

Kwa Maelezo Zaidi:

Tanzania:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dar es Salaam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744

Kenya:
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi Kenya Simu: +254222111031

Kimechapwa na Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salaam, Tanzania / Nairobi, Kenya

ISBN: 978-1-83596-500-9
10 9 8 7 6 5 4 3 2 1

Neno la Mwenezi

Kazi nyingine ya Dawati la Kiswahili imo mikononi mwenu, ndiyo tafsiri ya *Ruidade Jalsae Du'aa* — Kumbukumbu za Mkutano wa Dua.

Hii ndiyo habari ya zama kabla ya Bara Hindi kupata uhuru. Siku hizo nchini India ilitawala serikali ya Kiingereza kwa kuuondolea mbali utawala wa mabavu wa Makalasinga. Serikali ya Masingasinga ilikuwa imewanyima wananchi uhuru wa dini. Mwadhini akitoa adhana kwa sauti ya juu akaadhibiwa vikali, hata kuuliwa. Ng'ombe akiwahi kupata dhara kidogo kwa bahati mbaya, mtu husika aliweza kukatwa mkono kama si kuuawa.

Seyidna Ahmad[as] aliwasihi Waislamu kuitolea shukurani serikali ya Kiingereza iliyoleta amani nchini na kila mtu alikuwa na uhuru wa kutekeleza maagizo ya dini yake.

Siku hizo nchi ya Transvaal (Jimbo la Afrika kusini) ilianza vita na serikali ya Kiingereza. Seyidna Ahmad[as] aliwahimiza waumini kuiombea serikali ushindi katika mapigano hayo. Na siku ya Idul Fitri iliyokuwa tarehe 2 Februari 1900, akatoa hotuba baada ya sala ya Idi iliyoongozwa na Maulana Maulawii Nurud Din[ra]. Waaminio elfu wa Qadian, vitongoji vyake, na wananchi wa Afghanistan, Iraki, Madras, Kashmir na wilaya mbalimbali za India walihudhuria kwa jazba kubwa.

Akihutubia wahudhuriao Seyidna Ahmad[as] akatoa maelezo ya Sura An-Naas, na akaeleza haki za Mungu pamwe na haki za watu, ambazo zote hizo zalazimika kutekelezwa.

Seyidna Ahmad[as] akafafanua agizo la Mwenyezi Mungu lililomo ndani ya Kurani Tukufu kwamba Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye madaraka kati yenu (An-Nisaa 4:60). Akaeleza kinaganaga kwamba hii haimaanishi watawala Waislamu tu, bali watawala wowote, hususan wale wafanyao hisani.

Akaeleza kwa utondoti habari za kiimla za Masingasinga na ukatili wao na kulinganisha na wema na hisani ya serikali ya Kiingereza, na akawahimiza waumini kuiombea serikali ushindi katika vita ya Transvaal. Hatimaye akaongoza dua kwa jazba na ikhlasi kwa serikali ya Kiingereza kupata ufaulu.

Isitoshe, waumini kwa kuelekezwa na Mwongozi Mtukufu wakachanga rupia 500 kwa majeruhi wa serikali katika vita hiyo na kuipelekea serikali.

Seyidna Ahmad[as] alipoisifu serikali ya Kiingereza kwa kuwaokoa Waislamu katika udhalimu wa Masingasinga, hakupaka mafuta kwa mgongo wa chupa. Kwani, yeye pia alipinga vikali itikadi za Wakristo juu ya Utatu, Kafara ya Yesu.

Siku hizi baadhi ya wapinzani wetu wanapinga Seyidna Ahmad[as] kuagiza kuitii serikali ya Kiingereza na kuitolea shukurani kuleta uhuru wa dini, lakini ni la kushangaza kwamba hao wapinzani baada ya kupata uhuru Bara Hindi wengi wao wanapenda sana kuhama nchi yao huru na kufika Uingereza kwa njia yoyote hata isiyo ya halali kwa kuishi chini ya utawala wa Waingereza!!

Twamshukuru Sheikh Khurram Shahzad kuchukua jukumu la kufasiri 'Kumbukumbu za Mkutano wa Dua' kwa Kiswahili. Kabla ya kuipeleka mtamboni nilidurusu kwa uangalifu ili kuisogeza karibu zaidi na matini ya Kiurdu. Sheikh Ansar Hussain alishughulikia kutengeneza fomati. Mwenyezi Mungu Awajalie wote hao wawili malipo bora.

Twatumai wasomaji watukufu watanufaika na kijitabu hiki, Mungu Akijalia.

Jamil R. Rafiq
Wakilut-Tasnif
Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan 24 Septemba 2024

ٹائیٹل بار اول

أَطِيعُوا اللّٰهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنْكُمْ

روئداد جلسہ دعا

جو حضرت سیدنا و امامنا عالیجناب میرزا غلام احمدؑ
صاحب مسیح موعود مہدی مسعود کی
تحریک پر دارالامان قادیان
میں بتاریخ ۲ فروری سنہ ۱۹۰۰ء
منعقد ہوا

مطبوعہ مطبع ضیاء الاسلام قادیان دارالامان

Tafsiri ya jalada la chapa ya kwanza

Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye madaraka kati yenu.

KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA DUA

Uliofanyika mjini Qadian, Darul Amaan mnamo
2 Februari 1900, kwa kuelekezwa
na Seyidina na Imamana
Ghulam Ahmad[as],
Masihi Mau'udi.

Kimechapishwa katika matbaa Dhia ul Islam,
Qadian Darul Amaan.

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ [1]   نَحۡمَدُہٗ وَنُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ [2]

Kumbukumbu za Mkutano wa Dua

Uliofanyika mjini Qadian, Darul Amaan
mnamo 2 Februari 1900, kwa kuelekezwa na
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as], Masihi Mau'udi.

Kabla hatujaweka kumbukumbu hizi mbele ya wasomaji, kwanza tunaona ni lazima kujulisha kuwa Mtukufu Imam wa wamchao Mungu, *Hujjatullahi* [hoja ya Mwenyezi Mungu duniani], Hadhrat Mtukufu Mirza Ghulam Ahmad chifu wa Qadian Masihi[as] wa Zama kama awatakiavyo heri mahuluku wote, vivyo hivyo alivyo mwaminifu na mwenye kuitakia heri serikali iliyopo kwa moyo wote. Ni dhati yake yenye baraka iliyodhihirisha kwa uwazi mno haki za raia na haki za serikali, na akajaza nyoyoni mwa Jumuiya yake shukrani kwa hisani za serikali hii yenye tajamala kwa njia mbalimbali na zenye kuathiri ambazo kwazo likafutika kila doa la unafiki kutoka katika mioyo ya Jumuiya hii tukufu kwa dola hili, hivi kwamba haikubaki hata alama yake. Hii ilikuwa tabia ile inayoshamiri baina ya Waislamu wasio na ujanja na wasiojua kwa sababu ya

---

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.

[2] Twamhimidia Yeye na kumsalia Mtume wake Mkarimu.

usuhuba wa masheikh wenye chuki na majahili. Na hawa wakawa waaminifu na wenye shukrani kwa serikali ya Kiingereza kwa moyo mkunjufu, kwa namna walivyotakiwa kuwa kwa serikali yoyote ya Kiislamu.

Halijafichika kwa serikali yenyewe pia kwamba ukoo wa Janabi Mtukufu umekuwa siku zote muaminifu na wenye kujitolea na katika masaibu umekuwa unaisaidia fauka ya uwezo wake. Kutokana na hilo viongozi wa serikali wanaweza kuamulia kwamba ukoo wa Janabi Mirza Mtukufu unao uhusiano wa itifaki na serikali hii. Ingawaje wazee wa Hadhrat mtukufu walikuwa wanaisaidia kwa wanajeshi na wapanda farasi, lakini yeye hakusahau kuisaidia kivyake kwa dua nyingi zenye uchungu sana. Basi, wakati wowote ule vilipotokea vita na mapigano mipakani mwa Afghanistan au Balochistan au Barma [Myanmar], yeye aliendelea kuiombea dua. Alifurahia sana jubilii ya Mhashamu Malkia Kaisari na kwa kufanya mkutano alimwombea umri mrefu na ustawi kwa Mwenyezi Mungu. Na katika hali yake hiyo ya maisha yaliyo ya udarweshi mtupu, na daima ameyapenda maisha haya ya upweke na upekee, mbali na kuomba dua anawezaje kuisaidia serikali yake yenye hisani na huruma. Basi, katika hafla hii pia akaonelea huyu mwenye kuwahurumia mahuluku kuiombea serikali ya Kiingereza ushindi inayoudhiwa pasipo haki na kundi la watu fulani linalosaidiwa kisiri-siri na

makundi mengine. Basi, mnamo Februari mosi Seyidina Ahmad[as] aliwaambia wanajumuiya wake waliokuwa wamewasili kutoka Afghanistan, Iraki, kutoka miji mbalimbali ya India kama vile Madras, Kashmir, Shahjahan Pur, Jammu, Mathra, Jhang, Multan, Patiala, Kapurthala, Maler Kotla, Ludhiana, Shahpur, Sialkot, Gujrat, Lahore, Amritsir, Gurdaspur wilaya kama hizi n.k., kwamba twapenda kuwa siku ya Idi tuiombee ufaulu serikali ya Kiingereza, na wote kwa kusikia wakaipenda kwa uchangamfu.

Basi, kwa sababu hii, siku ya Idi zipatazo saa mbili asubuhi, Hadhrat Masihi Mau'udi[as] pamwe na Jumuiya yake alielekea uwanja mkubwa ule uliopo upande wa magharibi wa kijiji cha Qadian, ambao pia ni uwanja wa zamani wa kusali Sala ya Idi. Na watu waliendelea kukusanyika hapo mpaka saa tatu kutoka vijiji vya mbali na karibu. Kisha, mwanazuoni wa dahari, wa pekee katika zama, Maulana Maulawi Hakim Nur-ud-Din alisalisha sala ya Idi. Na baada ya sala Mtukufu Hadhrat Imam wa Zama akiinuka alihutubia kwa ufasaha na balagha kubwa. Hotuba ilikuwa yenye athari kubwa kiasi hiki kwamba watu wote wasiopungua elfu walitega masikio vizuri; na ilikuwa bayana na rahisi kueleweka kiasi hiki kwamba hata washamba wasiostaarabika wakapata kusema kwa kuvutika kwamba ni kweli kabisa ayasemayo Hadhrat Mtukufu. Katika hotuba hii,

itakavyobainika kutokana na hotuba yenyewe, pamoja na haki za Mwenyezi Mungu, namna zilivyoelezwa kinagaubaga haki za viongozi wa utawala, na jinsi raia walivyojulishwa kuwa serikali hii ya Kiingereza imetufanyia sisi Waislamu hisani nyingi kiasi gani, na sisi Waislamu tumelazimishwa kiasi gani kwa mujibu wa Kurani Tukufu kuwa na uaminifu na kujitolea kwa serikali. Je yupo mtu duniani awezaye kuthibitisha kulingana na dini, haki za serikali ya Kiingereza kwa dhati ya moyo na nia njema. Hii ni kazi ya huyu shujaa ambaye ameshatilia nyoyoni mwa Jumuiya yake upendo wa kweli kwa serikali. Na mara kwa mara akaisistizia Jumuiya yake kwa maandishi na hotuba kuwa yeyote miongoni mwenu akionesha unafiki hata sawa na punje ya haradali kwa serikali yake, yeye hatahesabiwa katika Jumuiya yetu na atakuwa mwasi wa Mwenyezi Mungu na Mtume[saw]. Kwani, sisi hatuisifu na kuitaadhimu serikali ya Kiingereza kwa manufaa binafsi au kwa ubinafsi, bali kwa mujibu wa dini ya Islam tunao wajibu wa kuonyesha uaminifu wetu kwa vitendo na maneno kwa usafi wa batini na moyo wa kweli. Twaona ni haramu kufanya hila za unafiki na kuisifu kwa kutia chumvi kupata lakabu au mashamba au ardhi. Kwa kuwa hotuba yenyewe ilivyo inaandikwa hapa chini, hivyo hatuna haja ya kusema zaidi.

HOTUBA

ya

Mtukufu Masihi Mau'udi, baraka na amani juu yake, iliyotolewa baada ya sala ya Idul Fitri

Waislamu wanapaswa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu Aliyewajaalia dini iliyotakasika kielimu na kimatendo, na kila aina ya ufisadi, mambo yakirihishayo na kila aina ya ubaya. Kama binadamu akitafakari kwa makini na uangalifu, atapata kujua kwamba kwa hakika Mungu Mwenye enzi pekee ndiye Anastahiki hamdu na sifa zote njema, na mwanadamu au mahuluku yeyote hastahiki hamdu na sifa kwa kweli na kwa hakika. Mtu akiona pasipokuwa na ubinafsi wa aina yoyote atadhihirikiwa kwa uwazi sana kwamba mtu anayestahiki hamdu, anaweza kustahiki ama kwa sababu yeye awe mwumba wa kiumbe fulani pindi ambapo hapakuwa na kiumbe chochote wala habari ya kiumbe chochote, au kwa sababu hii kwamba katika zama ambapo hapakuwa na kiumbe chochote wala haikujulikana kwamba kwa ajili ya uwepo wa kiumbe na kubaki kwake, usalama wa afya na kukimu maisha, vifaa gani vinalazimu kuwepo, naye awe ameishaweka tayari hivyo vyote, au katika zama ambapo matatizo mengi yangeweza kumsibu huyo kiumbe na yeye awe amemrehemu, na kumhifadhi. Au mtu anaweza

kustahiki sifa kama asipoteze juhudi ya mfanya jitihada, na awatolee kikamilifu haki za wafanya jitihada. Ingawaje kidhahiri kutoa haki za wafanya jitihada ni ujira, lakini mtu yule pia anaweza kuwa mhisani anayetoa haki barabara. Sifa hizo ni za daraja ya juu ziwezazo kumfanya mtu kustahiki hamdu na sifa. Sasa, angalieni kwa kuzingatia kuwa Mwenyezi Mungu pekee Mwenye sifa hizi kikamilifu ndiye kwa hakika Anastahili hamdu hizo zote, minghairi Yake yeyote hana sifa hizo.

Kwanza: Angalieni sifa ya kuumba na kulea. Kuhusu sifa hii mtu anaweza kufikiri kuwa wazazi na wahisani wengine wanakuwa na malengo na makusudio ambayo kwa sababu yake wanafanya hisani. Na dalili juu yake ni hii kuwa, mathalani, mtoto akizaliwa mwenye afya, mwenye sura nzuri na mwenye nguvu hapo wazazi wanapata furaha. Na akiwa mtoto wa kiume, furaha inakuwa maradufu. Inasherehekewa kwa shangwe na vigelegele. Lakini akiwa mtoto wa kike nyumba hiyo inakuwa kama mahali pa huzuni na siku hiyo inakuwa siku ya maombolezo, na wanaona aibu sana kuonana na wengine, pengine baadhi ya wapumbavu wanawaua watoto wa kike kwa njia mbalimbali au wanazingatia kidogo ulezi wao. Na lau mtoto akizaliwa kiwete, kipofu, mlemavu, wanatamani angekufa, na si ajabu pengine wanamuua wenyewe mara nyingi kwa kumwona ni msumbufu. Nimewahi kusoma kuwa

Wagiriki walikuwa wanawaua makusudi watoto kama hao, bali kwao ilikuwa ni kanuni ya kifalme kwamba mtoto yeyote akizaliwa mpungufu, mlemavu, kipofu n.k., basi huyo mara moja auawe. Hii yaonesha wazi kwamba katika fikara za kibinadamu huchanganyika makusudio yake ya kidhati na ubinafsi pamwe na kulea na kutunza; lakini Mwenyezi Mungu Hana makusudio yake ya kibinafsi katika uumbaji na ulezi wa mahuluku wengi hivyo (ambao kuwaza na kueleza, fikara na ulimi hushindwa, waliojaa kote ardhini na mbinguni). Yeye Hahitaji huduma na riziki kama wazazi, bali Amewaumba mahuluku kwa hamu ya kuwakimu. Kila mtu atakubali kwamba kupanda mmea kisha kumwagilia na kuutunza na kuuhifadhi hadi uwe mti wa kuzaa matunda ni hisani kubwa. Basi, mkitafakari juu ya mwanadamu, hali yake na kumkimu, itajulikana kuwa Mwenyezi Mungu Amemfanyia hisani kubwa kiasi gani kwamba katika mageuko mengi kiasi hicho, nyakati za unyonge na mabadiliko ya aina aina Amemsaida.

Jiha ya pili niliyoeleza hivi punde kwamba kabla ya kiumbe kuhulukiwa maandalio yawe hivi kuwa mahitaji yote yawepo kwa ajili ya maisha ya kijamii na kwa vipawa kufanya kazi vizuri. Angalieni, tulikuwa hatujazaliwa bado, Naye Akatoa mahitaji yote mapema. Jua ling'aalo lililoishachomoza tayari saa hizi, na kwalo mwanga umeenea kote na upo mchana, kama

lisingekuwepo, je tungeweza kuona? Au kupitia mwanga faida na manufaa yanayoweza kupatikana kwetu, tungeweza kupata kwa njia gani? Kama jua na mwezi au mwanga wa aina yoyote ile usingekuwapo, uwezo wetu wa kuona ungekuwa bure. Ingawa macho yanayo nguvu ya kuona lakini pasipokuwa na mwanga wa nje, hiyo haifai kitu. Basi, ni hisani nyingi kiasi gani kwamba kwa kunufaika na vipawa, Alijalia mahitaji hayo muhimu mapema. Tena ni rehema Yake kiasi gani kuwa Ametujaalia nguvu za namna hii, na Ameziwekea vipawa visivyodhihirika ambvyo ni vya lazima kwa mwanadamu kukamilika na kufikia makusudio. Katika ubongo, neva, na mishipa Ameweka vipawa vya namna hii kwamba mtu anavitumia ipasavyo na anaweza kuvikamilisha, kwani Amewaumbia pia pamwe maandalio ya kuvikamilisha vipawa. Hii ni hali ya mfumo wa ndani kwamba kila kipawa kinaendana na utashi na manufaa ambamo mna ustawi wa mtu. Na kwa nje pia Ameweka utaratibu hivyo hivyo kwamba sawa na ufundi wa kila mtu alionao, Amemwekea sambamba nao vifaa na zana za kufaa hata kabla ya uwepo wake. Kwa mfano, mtu anayetengeneza viatu akiona ngozi na uzi huwa havipo, atavipataje na kwa njia gani ataweza kukamilisha ufundi wake; vile vile fundi cherehani asipopata kitambaa atashonaje? Vivyo hivyo ni hali ya kila mtu; tabibu hata akiwa hodari na

mjuzi namna gani, lakini kama dawa zenyewe hazipo, yeye anaweza kufanya nini? Ataandika dawa fulani kwa kutafakari na uangalifu mkubwa lakini dawa isipopatikana madukani atafanyaje? Fadhili ya Mwenyezi Mungu i kubwa kiasi gani kwamba kwa upande mmoja Amemjalia mtu elimu na kwa upande mwingine Ameumba mimea, vitu visivyo na uhai, na viumbe wenye uhai vinavyohitajika sawa na hali ya wagonjwa, na Ameviwekea sifa mbalimbali zinazoweza kusaidia katika kila zama sambamba na haja zisizotarajiwa. Ilmuradi, Mwenyezi Mungu Hakukiumba kitu kisichokuwa na faida. Imeandikwa katika vitabu vya utibabu kuwa mtu asipoweza kukojoa, baadhi ya wakati kwa kutia chawa kwenye ureta, mkojo unaanza kupita. Mwanadamu anafaidika kiasi gani na vitu hivyo, je mtu anaweza kukisia? La hasha! bali hawezi hata kuwaza. Halafu, jambo la nne ni malipo ya juhudi; hili nalo pia linahitaji fadhili ya Mwenyezi Mungu. Mathalani, mtu anajibidiisha sana akalima na kupanda mbegu, lakini kama usipokuwa msaada wa Mwenyezi Mungu, anawezaje kuleta nafaka nyumbani kwake? Kwa fadhili na ukarimu Wake tu kila kitu kinakuwa kwa wakati wake. Watu walikuwa karibu kuangamia katika ukame huu, lakini Mwenyezi Mungu Ameleta mvua kwa fadhili Yake tu na kuiokoa sehemu kubwa ya mahuluku. Ilmuradi, Mwenyezi Mungu kwanza kabisa

Anastahiki binafsi kuhimidiwa kikamilifu na kwa hali ya juu, mbele Yake hakuna yeyote anayestahiki kitu binafsi. Kama mtu mwingine anastahiki kutukuzwa, basi ni kwa kujaliwa Naye. Hii pia ni rehema ya Mwenyezi Mungu kwamba ingawaje Yu Mmoja Asiye na mshirika, lakini kwa hisani na huruma Yake Amewashirikisha baadhi yao katika sifa Zake, kama vile katika Sura hii tukufu Amesema:

قُلْ اَعُوْذُ بِرَبِّ النَّاسِ ۝٢ مَلِكِ النَّاسِ ۝٣ اِلٰهِ النَّاسِ ۝٤ مِنْ شَرِّ الْوَسْوَاسِ ۙ۬ الْخَنَّاسِ ۝٥
الَّذِىْ يُوَسْوِسُ فِىْ صُدُوْرِ النَّاسِ ۝٦ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ ۝٧ [3]

Humo Mwenyezi Mungu Amedokeza juu ya mstahiki sifa kwa muda mfupi pia pamwe na mstahiki wa sifa kwa hakika; na hii ndiyo ili hulka njema zipate kukamilika. Kwa hiyo, katika Sura hii Ametaja haki za aina tatu. Kwanza Amesema mjikinge kwa Allah Ambaye Anazo sifa zote njema kikamilifu, na Ambaye ni Mlezi wa watu. Na pia ni Mmiliki, na ni Mwabudiwa na Makusudio wa kweli. Hii Sura ni ya namna hii ambayo ndani yake tauhidi halisi imedumishwa, lakini papo hapo imeashiriwa pia kwamba msivunje haki za watu wengine walio dhihirisho la majina hayo kama kivuli. Katika neno la ***Rabb*** [Mlezi] imeashiriwa kwamba japo Mwenyezi Mungu Ndiye Mlezi hasa kwa hakika na ndiye Mfikishaji kwenye ukamilifu, lakini kwa kujaliwa

---

[3] An-Naas 114:2-7

na kama kivuli wapo wawili wengine walio dhihirisho la ulezi: mmoja kimwili na mwingine kiroho. Kimwili ni wazazi na kiroho ni kiongozi na mwongozi.

Sehemu nyingine Ametaja kwa kirefu pia:

وَقَضٰى رَبُّكَ اَلَّا تَعْبُدُوْٓا اِلَّآ اِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ اِحْسَانًا[4]

Yaani, Mungu Ametaka kuwa msimwambudu yeyote mwingine, na mfanye hisani kwa wazazi. Kwa hakika ni malezi mema namna gani kwamba mwanadamu anakuwa mtoto mchanga asiye na nguvu yoyote, katika hali hii mama anamhudumia kwa namna namna, na baba katika hali hiyo anamsaidia mama namna gani katika shuguli hizi ngumu. Mwenyezi Mungu kwa fadhili Yake pekee Ameandaa njia mbili kwa ajili ya ulezi wa kiumbe dhaifu, na kutoka katika nuru Zake za mapenzi Amewatilia ndani mwao mwale mmoja wa upendo Wake. Lakini ikumbukwe kwamba mapenzi ya wazazi siyo ya asili, bali yatiliwa ndani mwao, lakini mapenzi ya Mwenyezi Mungu ndiyo ya asili na maadamu hayatiliwi nyoyoni kutoka kwa Mwenyezi Mungu, mtu yeyote, akiwa ni rafiki au wa daraja moja, au mtawala, hawezi kumpenda yeyote. Na hii ni siri ya ulezi mkamilifu wa Mungu kwamba wazazi wanawapenda watoto sana mno hivi kwamba katika kuwatunza wanavumilia kila aina ya udhia kwa moyo

[4] Banii Israaiil 17:24

mkunjufu, hata kwamba hawajali kufa kwa uhai wao. Basi, kwa kukamilisha khulka njema Mwenyezi Mungu Ameashiria katika neno رَبِّ النَّاسِ [Mlezi wa watu] kwenye wazazi na mwongozi ili kwa mfululizo wa shukurani ya kimajazi na dhahiri, wapige hatua katika kumtolea shukrani Mola na Mwongozi wa asili. Na ufunguo wa kufungua siri hiyo ni kwamba Ameanza Sura hii tukufu kwa رَبِّ النَّاسِ [Mlezi wa watu]; Hakuanzisha na اِلٰهِ النَّاسِ [Mwabudiwa wa watu]. Kwani, mwongozi wa kiroho analea kulingana na matakwa ya Mungu Mwenye enzi kwa kuwezeshwa na kuongozwa na Mwenyezi Mungu, ndiyo sababu yeye pia amejumuishwa humo. Tena kipande cha pili ndani yake ni مَلِكِ النَّاسِ [Mfalme wa watu], yaani mjikinge kwa Mungu Aliye Mfalme wenu; na hii ni ishara moja nyingine ili watu wajulishwe kanuni ya dunia iliyostaraabika, na wastaarabishwe. Kwa hakika, Mwenyezi Mungu tu ndiye Mfalme, lakini ndani yake mna ishara kwamba kikivuli wanakuwepo wafalme. Kwa hiyo pia humu imedokezwa kuzingatia haki za mfalme wa wakati. Hapa panamaanisha mfalme kafiri, mshirikina au mwenye imani ya Umoja wa Mungu, yaani hamna sharti kama mfalme awe wa aina gani, bali ni mfalme tu japo awe wa dini yoyote ile; habari za dini na itikadi zimetengwa. Ndani ya Kurani popote Mwenyezi Mungu Alipomtaja mhisani, Hakuweka sharti kuwa awe Mwislamu na awe mwenye imani ya Umoja wa Mungu

na awe kutoka dhehebu fulani, bali imeelezwa kuhusu mhisani tu kwa ujumla, hata akiwa mwenye dini yoyote ile. Tena, Mwenyezi Mungu katika Neno Lake Tukufu Anasisitiza mno kumtendea mhisani kwa hisani, kama inavyobainika kutokana na aya ifuatayo:

هَلۡ جَزَآءُ الۡاِحۡسَانِ اِلَّا الۡاِحۡسَانُ [5]

Je malipo ya hisani yaweza kuwa tofauti na hisani?

Sasa, tunawajulisha kwa uwazi na wadhiha wanajumuiya wetu na wasikilizaji wote kwamba serikali ya Kiingereza ni mhisani wetu, imetufanyia hisani kubwa kubwa. Aliye na umri wa miaka 60 au 70 atakuwa anajua vyema kwamba zimepita zama za utawala wa Masingasinga juu yetu, wakati ule mateso waliyopata Waislamu hayafichikani; kuyakumbuka mwili unaanza kutetemeka na moyo hutetema. Wakati huo Waislamu walizuiwa kutekeleza ibada na wajibu wa dini ambavyo kuvitekeleza wanapenda zaidi kuliko hata uhai wao. Adhana ya sala iliyo utangulizi wa sala, kuitoa kwa sauti ya juu ikakatazwa. Kama mtoa adhana kwa kughafilika akitamka Allahu Akbar kwa sauti ya juu, akauawa. Kadhalika mambo ya Waislamu kuhusu halali na haramu yaliingiliwa isivyotakikana. Katika kesi moja kuhusu ng'ombe, Waislamu maskini elfu tano waliuawa. Ni tukio la mjini Batala kuwa Sharifu mmoja mkazi wa

[5] Ar-Rahmaan 55:61

hapo aliporudi mlangoni pake kutoka nje, pale palikuwapo kundi la ng'ombe, akawasogeza kidogo tu kwa ncha ya upanga, kwa bahati mbaya ngozi ya ng'ombe mmoja ikapata kukwaruzwa kidogo, maskini huyu akakamatwa ikasisitizwa kuwa auawe. Hatimaye, baada ya maombezi mengi akaachwa kuuawa, lakini mkono wake lazima ukakatwa. Walakini angalieni, sasa watu wa kila taifa na dini wanao uhuru namna gani? Twawataja Waislamu tu. Serikali imetoa uhuru kamili wa kutekeleza wajibu wa dini na ibada. Na hadhulumiwi yeyote bure kuhusiana na mali, uhai na heshima yake, kinyume na zama zile zenye fitina ambapo mtu licha ya kuwa maasumu kiasi gani alikuwa anahofia kuhusu uhai na mali yake. Hivi sasa, ni jambo jingine kama mtu akiharibu mienendo yake na kustahiki mwenyewe adhabu kutokana na mienendo mibaya, maadili mabaya, na kwa kutenda uhalifu. Au mwenyewe kwa itikadi mbaya na mghafiliko akilegea katika ibada ni jambo jingine; lakini kutoka kwa serikali upo uhuru kamili wa kila aina. Leo mkitaka kuwa wenye ibada kiasi chochote mwaweza, hamna kizuizi. Serikali yenyewe inayaheshimu majumba ya ibada na kwa ajili ya ukarabati wake n.k. hutumia maelfu ya rupia. Kinyume chake katika zama za utawala wa Kisingasinga, hali ilikuwa kwamba bangi ilikuwa inasagwa misikitini na farasi kufungwa humo, mfano wake upo hata hapa

Qadian, na katika miji mikubwa ya Panjab mifano yake mtakuta kwa wingi mno. Mjini Lahore hadi leo misikiti mingi ipo mikononi mwa Masingasinga. Leo, kinyume chake, serikali ya Kiingereza inayaheshimu majumba haya matakatifu kwa kila namna ipasavyo. Na kufahamu kuheshimu nyumba za dini, miongoni mwa wajibu wake, kama vile siku hizi hizi Mheshmiwa Kaimu mfalme Lodi Karzon [Lord Curzon], amehakikisha kwa kitendo chake kukataa kuingia Msikiti Mkuu wa Delhi, kwa kuvaa viatu na kutoa mfano wa kuigwa wa hulka njema za kifalme. Na kwa hotuba alizozitoa mara kwa mara mahali mbalimbali imebainika namna anavyo-heshimu nyumba za ibada. Kisha angalieni kwamba serikali haikutangaza popote pale kuwa mtu asitoe adhana kwa sauti au asifunge saumu; bali imetoa kila anuwai za chakula — jambo ambalo hata alama yake haikuwapo katika zama mbovu za Masingasinga. Barafu, soda, biskuti, mkate n.k. kila anuwai za chakula ikaleta, na kutoa suhula ya kila aina. Huu ni msaada wa ziada uliozifikia desturi za Islam kutoka kwa watu hao. Sasa, kama mtu mwenyewe asifunge saumu ni jambo jingine. Ni la kusikitisha kwamba Waislamu wenyewe wanapuuzia sheria. Basi, angalieni kwamba waliofunga saumu siku hizi hawajakonda hata kidogo, na walioupitisha mwezi huu kwa kudharau hawajanenepa. Wakati wao pia umepita na zama za hawa pia. Zilikuwa

ni saumu za kipupwe, yalikuwa mabadiliko tu ya nyakati za kula; badala ya kula chakula saa moja au mbili ni kukila saa kumi au kumi na moja. Licha ya urahisi kiasi hiki, wengi hawakuheshimu desturi zilizoagizwa na Mwenyezi Mungu, na wakauhakirisha mwezi wa Ramadhani ulio mgeni mheshimiwa wa Mwenyezi Mungu. Kuja kwa Ramadhan katika miezi yenye urahisi hivyo ilikuwa kigezo cha aina fulani. Na saumu hizi zilikuwa kipimo cha kupambanua baina ya mtii na mwasi. Mintarafu ya Mwenyezi Mungu serikali imeshatoa uhuru wa kila namna. Matunda na maakuli ya aina aina hupatikana. Hakuna njia za naima na raha zisizoweza kupatikana leo. Hata hivyo, agizo lilipuuzwa; sababu yake ni nini? Ndiyo hii tu kwamba imani haijabaki mioyoni. Ole wao! Mungu Haheshimiwi hata sawa na topasi, kana kwamba wanafikiri hawatakutana na Mungu abadani wala hawatakabiliana Naye, wala hawatahudhuria mbele ya mahakama Yake. Laiti wakanao wangefikiri na kutaamali kwamba yapo mathibitisho ya uwepo wa Mwenyezi Mungu zaidi ya mwanga wa majua mamilioni. Ni la kusikitisha kwamba kwa kuona kiatu inaaminiwa kwa yakini kwamba yupo mtengenezaji wake, lakini ni bahati mbaya mno kwamba hata kwa kuona mahuluku wa Mwenyezi Mungu wasiohesabika, imani juu Yake isiwepo au iwe imani ya namna iliyo sawa na kutokuwa na imani. Rehema za

Mwenyezi Mungu zi tele mno juu yetu, mojawapo ya hizo ni kwamba Ametuokoa kutoka katika tanuri liwakalo. Zama za Masingasinga zilikuwa ni tanuri la moto, na ujio wa Waingereza ni ujio wenye rehema na baraka. Nimewahi kusikia kuwa mwanzoni Waingereza walipofika, mwadhini fulani huko Hushiarpur alitoa adhana kwa sauti ya juu, kwa kuwa ulikuwa ni mwanzo tu, na fikara ya Mabaniani na Masingasinga ilikuwa kwamba hata hao pia watazuia kutoa adhana ya sauti kubwa, au mithili yao kama ng'ombe akijeruhiwa na mtu watakata mkono wake, wakamkamata yule mwadhini aliyetoa adhana kwa sauti ya juu. Kundi kubwa wakampeleka mbele ya Naibu Kamishna. Wakakusanyika machifu na matajiri wakubwa wakubwa na wakasema, Mheshmiwa! unga wetu umechafuka, vyombo vyetu vimenajisika. Maneno haya alipoambiwa yule Mwingireza, yeye alistajaabu sana kwamba je adhana ina athari ya kunajisisha vitu vya kula? Akamwambia karani mkuu kuwa haipasi kufungua kesi hii hadi tajriba haijafanywa. Hivyo basi, akamwagiza yule mwadhini, katoe tena adhana ulivyotoa. Yeye akaogopa isije hiyo ikawa kosa la pili; akasita kidogo kutoa adhana; lakini alipotulizwa, akatoa adhana kwa sauti kubwa alivyokuwa ametoa. Mheshimiwa huyo akasema, sisi hatukudhurika nayo hata kidogo. Akamwuliza karani mkuu, je wewe umepata madhara

yoyote? Naye pia akasema kuwa hakupta madhara yoyote kwa hakika. Hatimaye akaachwa na kuambiwa, nenda katoe adhana upendavyo. Allahu Akbar. Huu ni uhuru kiasi gani, na hisani nyingi kiasi gani ya Mwenyezi Mungu. Kama kwa hisani hii na neema hii wadhiha, moyo usipohisi hisani ya serikali ya Kiingereza, basi moyo huu hauna shukrani, si mwaminifu na unastahili kutolewa kwa kupasua kifua na kutupwa.

Hata katika kijiji chetu hiki palipo msikiti wetu, kulikuwa na eneo la maafisa wa serikali. Huo ulikuwa wakati wa utoto wetu, lakini nimesikia kwa watu wenye kuaminika kwamba Waingereza walipokwisha pata utawala, kwa siku chache, kanuni ile ile ya zamani ilifuatwa. Siku hizo afisa mmoja alikuwa amekuja huku, aliyekuwa na askari mmoja Mwislamu, ambaye akaingia msikitini na kumwambia mwadhini kutoa adhana. Akatoa adhana akiogopa kwa sauti ndogo kama vile kunong'ona. Askari akamwuliza, je watoa adhana hivi? Mwadhini akasema, naam tunatoa hivyo hivyo. Askari akamwambia, hapana panda juu ya paa ukatoe adhana kwa nguvu zote uwezavyo, yeye akaogopa; hatimaye kwa kusisitizwa sana na yule askari akatoa adhana kwa sauti kubwa. Hapo Mabaniani wote wakakusanyika na kumkamata sheikh mwadhini. Maskini huyo akaogopa na kuhangaika kuwa afisa wa serikali atamnyonga; askari akamwambia mimi nipo pamoja nawe. Mabarahman

wakatili wakampeleka mbele ya yule afisa wa serikali, na kusema Bwana mkubwa, huyu ametuchafua. Afisa alikuwa anafahamu kuwa utawala umeshabadilika, na haupo tena ule wa Kisingasinga, lakini akamwuliza kwa sauti ndogo, kwa nini umetoa adhana kwa sauti ya juu? Askari akijitokeza mbele, akasema, si yeye nimetoa adhana mimi. Afisa akasema, Enyi wenye bahati ndogo! kwa nini mnapigia kelele, kule Lahore kwa sasa ng'ombe wanachinjwa hadharani, mnaililia adhana, kaeni mkiwa kimya. Ilmuradi, ni jambo la hakika hili na kweli linalotoka moyoni mwetu. Tusipowashukuru walio-tuokoa katika tabaka la chini la udongo, hiyo tena itakuwa kinyume na shukrani na kukosa uaminifu.

Mbali na haya, ujahili ulikuwa umeenea mno katika Panjab. Mzee mmoja, Kamme Shah, alisimulia kuwa nilimwona mwalimu wangu akiomba kwa uchungu sana wa hali ya juu kwamba lau angepata bahati ya kuiona **Sahihi Bukhari** mara moja. Na baadhi ya wakati kwa kufikiri inawezekanaje kuiona, alikuwa akilia sana akiomba dua mpaka kumamia. Na sasa Bukhari hiyo hupatikana Amritsar na Lahore kwa rupia mbili au nne. Kulikuwa na sheikh mmoja, bwana Sher Muhammad, yeye aliwahi kupata kurasa mbili tatu za **Ihya'ul 'Uluum;** kwa muda mrefu baada ya kila sala alikuwa akiwaonyesha wajao kusali kwa furaha na fahari kwamba hiki ni Ihya'ul 'Uluum, na alikuwa na

kiherehere sana kuwa angepata kutoka popote Ihya'ul 'Uluum nzima. Kwa sasa Ihya'ul 'Uluum iliyochapishwa inapatikana kila sehemu. Ilmuradi, kwa baraka ya ujio wa Uingereza jicho la kidini la watu limepata kufumbuka pia, na Mwenyezi Mungu Anajua vizuri kwamba kupitia utawala huu dini imepata kuauniwa kiasi gani kwamba haiwezekani katu katika dola jingine. Kwa baraka ya matbaa, na kwa uvumbuzi wa karatasi za aina aina, vitabu vya kila aina vinaweza kupatikana kwa bei ndogo ndogo, na kwa njia ya posta vinafika toka pahali popote kwenye mahali pengine nyumbani mwenu. Ndivyo njia ya kuhubiri kweli za dini imekuwa nyepesi na rahisi na safi sana. Halafu miongoni mwa baraka nyingine zilizopatikana kusaidia dini katika zama za serikali hii, mojawapao ni hii pia kwamba nguvu za akili na uwezo wa ufahamu umepata kuzidi. Halafu kwa sababu serikali imeipatia kila kaumu uhuru wa kueneza dini yake, kwa hiyo watu wamepata fursa ya kuchunguza mafundisho na hoja za kila dini na kuzitafakari. Watu wa dini mbalimbali walipoishambulia Islam ndipo Waislamu wakapata nafasi ya kutaamali juu ya vitabu vyao vya kidini kwa kuisaidia dini yao na kuisadikisha. Na nguvu zao za kiakili zikapata kuzidi. Ni jambo la kawaida kwamba kama vile nguvu za kimwili zinavyopata kuzidi kwa mazoezi, ndivyo hivyo nguvu za kiroho nazo pia hukua kwa mazoezi. Kama vile farasi anavyoenda

vizuri akipandwa na mpanda hodari, ndivyo hivyo kwa ujio wa Waingereza ilivyopatikana fursa ya kutafakari mafundisho ya dini, na wazingatiao wamepata uimara na nguvu ndani ya dini yao ya kweli. Na popote pale wapinzani wa **Kurani Tukufu** walipoleta upinzani, papo hapo wafikiriao wakapata hazina ya maarifa. Na kutokana na uhuru huu, elimu ya thiolojia ya chuo imepata maendeleo belele, na maendeleo haya yamekuwa hasa mahali hapa. Sasa, Mrumi au Msiria, hata awe msomi na mwanazuoni namna gani, akija hapa atashindwa kujibu vya kutosha shutuma za Wakrito na Waariya, kwani yeye hajapata nafasi ya kuyalinganisha mafundisho ya dini mbalimbali kwa uhuru na wasaa huu. Ilmuradi, kama vile amani ya kimwili imepatikana nchini kwa sababu ya serikali ya Kiingereza, ndivyo amani ya kiroho nayo ikapata kuenea kikamilifu. Kwa kuwa tunahusiana na mambo ya dini na ya kiroho tu, kwa hiyo tutataja zaidi mambo yale tuliyosaidiwa na serikali kama hisani kwa kutekeleza faradhi za dini. Basi, ikumbukwe kwamba mtu anaweza kufanya ibada kwa uhuru kamili na utulivu pale tu ambapo masharti manne yapatikane ndani yake, nayo ni haya:

La kwanza: Afya. Kama mtu akiwa dhaifu kiasi hiki kwamba hawezi hata kuinuka kutoka kitandani, huyu anawezaje kuzingatia barabara sala na saumu, na kadhalika atashindwa kutekeleza mambo mengi ya

lazima kama hija, zaka n.k. Basi, yatupasa kutafakari kwamba kwa sababu ya serikali tumepata kiasi gani njia za kutunza afya ya kimwili. Katika kila jiji na mji hospitali ya ngazi yoyote lazima inapatikana panapotibiwa wagonjwa kwa upendo na huruma; dawa na chakula vinatolewa bure. Baadhi ya wagonjwa kwa kulazwa hospitalini wanatunzwa na kuhudumiwa vizuri kiasi hiki kwamba mtu hawezi kugangisha kwa urahisi hivyo, suhula na raha hata nyumbani mwake. Idara moja imewekwa tofauti kwa utunzaji wa afya, inayogharimu mamilioni ya rupia kila mwaka. Hatua nyingi zimechukuliwa kwa ajili ya usafi wa vijiji vikubwa, miji na majiji. Kuna mipango mingine kwa kuondoa maji machafu na takataka zinazodhuru afya. Halafu dawa za kila aina zenye kuathiri haraka zinaandaliwa na kutolewa kwa bei nafuu, hata kwamba mtu anaweza kutibu inapohitajika kwa kuweka baadhi ya dawa nyumbani mwake. Elimu ya utibabu imeenezwa sana kwa kuanzisha vyuo vikubwa vikubwa vya matibabu hata kwamba madaktari wanapatikana vijijini pia. Kwa kuzuia na kuponya maradhi kadha ya hatari kama vile ndui, kipindupindu, tauni n.k. hasa kwa tauni siku hizi, hatua serikali ilizochukua zinastahili kushukuriwa sana. Ilimurudi, serikali imetoa kila aina ya msaada wa lazima kuhusiana na afya; na hivyo kwa kutimiza sharti la kwanza na la lazima kwa kutekeleza ibada imesaidia sana.

Sharti la pili ni Imani. Kama imani juu ya Mwenyezi Mungu na maamrisho Yake imekosekana, na ndani kwa ndani ukoma wa kutokuwa na dini na ukanaji wa dini umemkumba, hapo pia maagizo ya Kiungu hayawezi kutekelezwa; ndiyo maana watu wengi wanasema ایہہ جگ مٹھاتے اگلا کن ڈٹھا [dunia hii tamu, nani ameiona Akhera]. Ni la kusikitisha kwamba kwa shuhuda ya watu wawili mhalifu anaweza kunyongwa, lakini licha ya ushahidi uliopo wa Manabii laki moja elfu ishirini na nne na Mawalii wasiohesabika, bado ukanaji wa aina hii haujaondoka nyoyoni mwa watu. Katika kila zama Mwenyezi Mungu kwa ishara Zake zenye nguvu na kwa miujiza Anasema أَنَا الْمَوْجُوْدُ , [Mimi Nipo], lakini hawa wenye bahati ndogo hawasikii ijapokuwa wanayo masikio. Ilmuradi, sharti hili nalo ni la lazima sana; kwa hiyo pia twapaswa kuishukuru serikali ya Kiingereza. Kwani, kwa kuimarisha imani na itikadi, elimu ya dini kwa watu wote ilikuwa inahitajika, na elimu ya kidini ilitegemea uenezaji wa vitabu vya dini. Kwa baraka ya matbaa na posta, vitabu vyote vya kidini vyaweza kupatikana, na kupitia magezeti nafasi ya kubadilishana mawazo nayo hupatikana. Watu wenye bahati njema wanayo fursa kubwa ya kujiimarisha kiimani na kiitikadi. Isitoshe, jambo lililo **la lazima**, na la lazima sana, kwa kuimarisha imani ni ishara za Mwenyezi Mungu zinazodhihirika kwa mkono wa mtu anayetumwa na

Mwenyezi Mungu, na kwa vitendo vyake anahuisha kweli na maarifa yaliyopotea. Basi, yapasa kumshukuru Mwenyezi Mungu kuwa Yeye Amemtuma mtu wa namna hiyo katika zama hizi kwa kuhuisha imani upya, na Amemtuma ili watu waongezeke katika nguvu ya yakini, aliyefika katika enzi ya serikali hii yenye baraka. Yu nani? Ndiye huyu anayeongea akisimama kati yenu. Kwa kuwa hili ni jambo lililokubalika kuwa mtu hawezi kutenda kikamilifu matendo mema hadi imani iwe imekamilika. Kadiri jiha fulani au kona za imani zitakazokuwa zimeanguka kadiri hiyo hiyo mtu atakuwa mzembe na mnyonge kwenye amali, ndiyo maana walii anaitwa yule ambaye kila jiha yake huwa imesalimika, na si dhaifu kwa jiha yoyote ile; ibada zake ziwe zafanyika kikamilifu kitimilifu. Alimradi, sharti la pili ni usalama wa imani.

Sharti la tatu kwa mwanadamu ni uwezo wa kifedha. Kujenga misikiti na kutekeleza mambo yahusuyo Islam hutegemea fedha. Isitoshe, maisha ya kijamii na mambo mengine yote, hususan kuendesha mambo ya misikiti huwa vigumu sana. Sasa, kwa jiha hii iangalieni serikali ya Kiingereza. Serikali imeiendeleza mbele sana biashara ya kila aina. Kwa kueneza elimu imewapa ajira wananchi, na wengine imewapa nyadhifa kubwa kubwa, na kwa kutoa njia za safari imesaidia kwenda nchi nyingine na kuleta fedha kwa kujichumia basi, angalieni

madaktari, mawakili, viongozi wa mahakama, wafanya-kazi wa idara ya elimu. Ilimradi, kwa njia nyingi watu wanajichumia rupia nyingi, na wafanyabiashara kwa bidhaa mbalimbali za biashara wanakwenda nchi za Ulaya, na nchi za mbali — Afrika Australia n.k. na wanarudi wakipata mali tele. Ilmuradi, serikali imefanya rahisi sana kupata ajira kwa watu wote, na kwa kujichumia fedha imetengeneza njia nyingi.

Sharti la nne ni Amani. Sharti hili la amani haliko ndani ya hiari ya mtu mwenyewe. Tangu dunia iumbwe, hiyo imechukuliwa kuwa ni jukumu la dola. Kadiri dola litakavyokuwa lenye nia njema na moyo wake utakuwa umetakasika na unafiki, kadiri hiyo sharti hili litatimia vizuri zaidi. Sasa, katika zama hizi, sharti la amani linatimia kwa hali ya juu kabisa. Nina yakini kamili kwamba mchana wa zama za Masingasinga ulikuwa mbaya kuliko mausiku ya zama za Kiingereza. Karibu hapa kuna kijiji cha Butar[6] ambapo kama mama mmoja alikuwa akienda huko kutoka huku akaenda kwa kulia kwa uchungu kuwa Mungu Anajua ataweza kurudi au la. Sasa, hali imekuwa hii kwamba mtu akienda hata mpaka mwisho wa ardhi, hakuna hatari kwake. Njia za safari zimefanywa rahisi sana kwamba raha ya kila namna ipo, kana kwamba mtu yupo nyumbani akiwa

[6] Kijiji hiki ni karibu maili mbili kutoka Qadian.

amekaa au amelala katika gari moshi na kufika popote apendapo. Ipo idara kubwa ya polisi kwa ajili ya usalama wa mali na uhai. Kwa kulinda haki, mahakama zi wazi, mtu aendelee hadi apendapo kupata msaada wa kisheria. Ni hisani nyingi kiasi gani zilizosababisha uhuru wetu kimatendo. Basi, katika hali ambapo hisani zisizo-hesabika zinafanywa juu ya mwili na roho, litakuwa ni jambo la kushangaza sana isipozalika jazba ya suluhu na shukrani ndani mwetu. Asiyewashukuru mahuluku, hawezi kumshukuru Mwenyezi Mungu pia. Sababu yake nini? Ni hii kwamba kiumbe huyo naye pia ni mjumbe wa Mwenyezi Mungu na anafanya sawa na matakwa ya Mwenyezi Mungu. Ilimradi, mambo haya yote niliyoeleza yanamlazimisha mtu mwenye moyo mwema kumshukru mhisani kama huyo. Hii hii ndiyo sababu twataja mara kwa mara katika vitabu vyetu na hotuba zetu hisani za serikali ya Kiingereza, kwani moyo wetu kwa hakika umejaa ladha ya hisani zake. Majahili wasio na shukrani wakikisia amali yetu hii isababishwayo na ukweli na ikhlasi kuwa ni kujikomba, sawa na tabia zao za kinafiki.

Sasa, nikirejea kwenye mada hasa tena, napenda kujulisha kwamba katika Sura hii kwanza Mwenyezi Mungu Amesema رَبِّ النَّاسِ , kisha مَلِكِ النَّاسِ . Na mwishoni Amesema اِلٰهِ النَّاسِ , Aliye kusudi na lengo hasa la mwanadamu. اِلٰه lamaanisha Mwabudiwa, kusudio,

shabaha. لَا اله إِلَّا اللهُ maana yake ndiyo hii kwamba لَا مَعْبُوْدَ لِيْ وَلَا مَقْصُوْدَ لِيْ وَلَا مَطْلُوْبَ لِيْ إِلَّا اللهُ [Hakuna mwabudiwa wangu wala kusudi wala shabaha yangu ila Allah]. Hii ndiyo tauhidi ya kweli kwamba Mwenyezi Mungu pekee Aaminiwe kustahiki kila hamdu na sifa. Halafu Amesema مِنْ شَرِّ الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ[7], yaani ombeni kujikinga na shari ya خَنَّاسِ atiaye wasiwasi. *Khannaas* kwa Kiarabu ni nyoka na kwa Kiibraniya ni نَحاش, kwani alifanya uovu kabla pia. Hapa Hakusema 'Iblisi' au 'shetani', ili mwanadamu apate kukumbuka jaribio lake la mwanzo kwamba namna gani shetani aliwadanganya wazazi wake. Wakati huo yeye aliitwa jina *Khannaas*. Utaratibu huu Mwenyezi Mungu Ameuweka ili Amjulishe mwanadamu matukio ya nyuma kwamba namna shetani alivyomfanya binadamu kwa kumdanganya asimtii Mungu, vivyo hivyo isije wakati mwingine akamfanya kuasi na kutomtii mfalme wa wakati. Na hivyo mwanadamu daima aendelee kuchunguza nia na makusudio ya nafsi yake kwamba kiasi gani anamtii mfalme wa wakati, na aendelee kujitahidi na kumwomba Mwenyezi Mungu dua kuwa shetani asipate kuingia ndani mwake kwa mlango wowote. Sasa, katika Sura hii agizo liliopo la utii, ndilo la utii wa Mwenyezi Mungu, kwani utii kwa hakika ni wa

[7] An-Naas 114:5

Kwake tu; lakini agizo la kuwatii wazazi, mwongozi na kiongozi na mfalme wa wakati pia Amelitoa Mwenyezi Mungu. Na faida ya utii itakuwa hii kwamba mtasalimika na kutiishwa na *khannaas*. Basi, ombeni kujikinga kuwa msalimike na shari ya kutiwa wasiwasi na *khannaas*, kwani mumini haumwi mara mbili kutoka katika shimo moja. Kwa njia mliyopata taabu, msijinase humo mara nyingine. Basi, katika Sura hii imeashiriwa kwa uwazi kumtii mfalme wa wakati. *Khannaas* Amewekewa sifa ndani yake vile Alivyoweka Mwenyezi Mungu sifa katika vitu kama vile miti, maji, moto n.k. na elementi. Neno عنصر [‘an-sar] kwa hakika ni عَنْ سِرٍّ [*an sirr*]. Katika lugha ya Kiarabu ص na س huwa zinabadilishana. Yaani, kitu hiki kimo katika siri za Mwenyezi Mungu. Kwa hakika kufika hapa utafiti wa binadamu unakoma. Ilimuradi, kila kitu hutoka kwa Mwenyezi Mungu, kikiwa ni aina ya mchangnyiko au si ya mchanganyiko. Basi, kama ni hivi kwamba kwa kuwatuma wafalme kama hawa Ametukomboa kutoka katika melfu ya matatizo, na Akatujalia badiliko kwamba kwa kututoa kutoka katika tanuri la moto Ametupeleka kwenye bustani ambapo pana mimea yenye kuburudisha, na kila upande vijito vinapita na upepo mwanana unavuma, basi itakuwa ni kutokuwa na shukrani sana kama mtu akisahau hisani Zake. Hasa

Jumuiya yetu iliyojaaliwa busara na Mwenyezi Mungu, nao kwa hakika hawana unafiki kwa hakika, yawapasa kuwa mfano bora wa kutoa shukurani, kwani yule waliyeungana naye, yeye hana unafiki hata sawa na chembe. Nina yakini kamili kwamba Jumuiya yangu haina unafiki, na busara yao haikukosea kujenga uhusiano nami, kwani kwa hakika mimi ndimi yule ambaye kwa ujio wake busara ya kiimani imeelekeza kuungana naye. Mwenyezi Mungu ni Shahidi na Anajua kuwa mimi ni yule mkweli, mwaminifu na Mau'udi ambaye ahadi yake ilitolewa na kinywa kitukufu cha Seyidna na Maulana, Mkweli na Aliyesadikiwa, Mtume Mtukufu[saw]. Nami nasema kweli kabisa kwamba wasioungana nami, wamejinyima neema hii. فِراسَة [busara] kana kwamba ni karama. Neno la فراسَة linatumika kwa fat-h ya ف na kwa kasr ya ف pia. Likitumika kwa fa-tha ya *Fa* maana yake ni kupanda farasi. Muumini anakuwa mpanda hodari nafsi yake kwa busara, anajaaliwa nuru na Mungu ambayo kwayo anapata mwongozo; ndiyo sababu Mtume Mtukufu[saw] alisema: اِتَّقُوْا فِرَاسَةَ الْمُؤْمِنِ فَإِنَّهُ يَنْظُرُ بِنُوْرِ اللهِ , yaani jihadharini na busara ya muumini, kwani yuangalia kwa nuru ya Allah. Ilimuradi, ushahidi mkubwa wa busara ya kweli ya Jumuiya yetu ndiyo hii kwamba wameweza kuitambua nuru ya Mungu. Hivyo basi, natarajia kwamba Jumuiya

yetu itapiga hatua kubwa kimatendo pia, kwani hiyo haina unafiki, nayo imetakasika na tabia ile ya wapinzani wetu ambao wakikutana na watawala wanawasifu, na wakirudi nyumbani wanawataja kuwa makafiri. Enyi wanajumuiya wangu, sikilizeni na kumbukeni kuwa Mwenyezi Mungu Hapendi tabia hii. Ninyi mnao uhusiano na mimi, na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu. Wafanyieni wema wafanyao wema, na wasameheni wafanyao uovu. Mtu hawezi kuwa mkweli hadi awe mnyofu. Mwenye mwenendo wa kinafiki, aliye kauleni, hatimaye anakamatwa. Kuna methali maarufu: دروغگو را حافظہ نباشد [mwongo ana kumbukumbu mbaya].

Hivi sasa, ningependa kunena jambo jingine muhimu nalo ni kwamba wafalme mara nyingi wanakabiliana na mapigano ambayo nayo pia yanakuwa tu kuwakinga na kuwalinda raia. Mmeshuhudia kuwa serikali yetu imelazimika kupigana mpakani mara kadhaa. Ingawaje watu wa mpakani ni Waislamu, lakini kwa mtazamo wetu hawako juu ya haki, kupigana kwao na Waingereza haijuzu kidini na kwa jiha yoyote ya dini, wala hawapigani kwa sababu ya dini kwa hakika. Je wanaweza kutoa udhuru kwamba serikali haijawapa Waislamu uhuru? Bila shaka, imewapa na imewapa kwa namna ambayo mfano wake hauwezi kupatikana kwa kuishi

kule Kabul na vitongojini mwa Kabul. Yasikika mambo ya Amiri [wa Kabul] siyo mazuri. Hakuna sababu ya majinuni hao wa mpakani kupigana ila kujaza tumbo. Wakipata rupia 20/30 tu, jazba yao ya kupigana kwa dini inatoweka. Hawa ni watu nduli na wanaharibu jina la Islam. Islam inaasisi haki za mfalme wa wakati na mhisani, watu hawa wenye tabia duni wanavunja mipaka ya Allah kwa tumbo lao. Na ithibati kubwa ya uduni na ujahili na ukatili wao ni hii kwamba kwa ajili ya chapati moja tu wanamwaga damu ya mtu kwa urahisi. Halikadhalika serikali yetu inakabiliana na nchi ndogo ya Jamhuri ya Transvaal, nchi hiyo siyo kubwa kuliko Panjab. Na huu ni upumbavu wake mtupu kuwa imeanzisha kukabiliana na nchi kubwa sana. Lakini, kwa kuwa yameshaanza mapigano, ni wajibu wa kila Mwislamu kuwaombea Waingereza ushindi. Tuna uhusiano gani na Transvaal? Aliyetufanyia maelfu ya hisani, ni faradhi yetu kumtakia heri. Hata jirani mmoja ana haki nyingi kiasi kwamba kwa kusikia tu taabu yake moyo unapata kulainika. Sasa, je kwa kusoma kuhusu masaibu ya wanajeshi waaminifu kwa serikali ya Kiingereza, moyo wetu hauhuzuniki? Kwangu mimi, yu mwenye moyo mgumu ambaye haoni shida za serikali kama shida zake. Kumbukeni, jedhamu ipo ya aina nyingi. Jedhamu moja inayousibu mwili unaitwa

ukoma, na jedhamu nyingine inayoisibu roho, inayomfanya mtu kupeketeka. Yaani, yaifurahia taabu ya watu; na kuhuzunika wakipata heri. Huku kwetu mtu mmoja wa aina hii alikuwa anaishi penye maduka; kama mtu fulani akifunguliwa mashtaka, akamuuliza hali ya kesi ikoje. Akiambiwa ameachiliwa au kesi inaendelea vizuri, huyu akaudhika sana, na kukaa kimya; kama akiambiwa kuwa ameshtakiwa rasmi, akafurahi sana kusikia kirefu habari yote kwa kumkalisha pamoja naye. Ilimuradi, baadhi ya watu wanayo tabia ya kuwatakia wengine ubaya kwamba wanataka kusikia habari mbaya, na wanaufurahia ubaya wa watu, kwani sera ya shetani huwa ndani mwao. Basi, haifai kumtakia mtu ubaya, hususani mhisani. Hivyo naiambia Jumuiya yangu kwamba isiige mfano wa watu wa namna hii, bali kwa huruma kamilifu kuitakia heri serikali ya Kiingereza waiombee ufaulu, na pia waoneshe mifano ya uaaminifu kwa vitendo. Hatusemi haya yote kwa kupata malipo au tuzo yoyote. Tunayo haja gani ya malipo, tuzo au lakabu za kidunia. Nia zetu Anazijua vyema Mungu Alimu kwamba kazi yetu yote ni kwa ajili Yake na ni kwa amri Yake. Yeye Ndiye Aliyetufundisha kumshukuru mhisani; kwa kutoa shukrani twamtii Mola wetu Karima, Naye tu twatarajia kuzawadiwa. Basi, ninyi mlio Jumuiya yangu, mwithamini sana serikali yenu mhisani.

Sasa, ningependa tufanye maombi kwa ajili ya vita ya Transvaal. Basi.

★★★

Baadaye Hadhrat Mtukufu alinyanyua mikono yake kwa jazba na ikhlasi kwa ajili ya kuomba, na wahudhuriao wote ambao idadi yao ilizidi elfu moja, waliomba dua, na kwa muda mrefu iliombwa dua kwa ajili ya ushindi na ufaulu. Baada yake Hadhrat mtukufu alipendekeza kwamba yalazimu kutuma mchango kwa ajili ya majeruhi wa serikali ya Kiingereza; na kwa ajili yake tangazo moja pia likachapishwa, nalo ndilo lifuatalo.

Mwandishi Mirza Khuda Bakhsh kutoka Qadian

Tangazo Moja la Lazima kwa Jumuiya yangu

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ   نَحْمَدُهٗ وَنُصَلِّيْ عَلٰى رَسُوْلِهِ الْكَرِيْمِ

Kwa kuwa serikali ya Kiingereza imewafanyia hisani kubwa kubwa Waislamu wa India kwa ujumla na hususani Waislamu wa Panjab, kwa hiyo Waislamu wakiishukuru serikali yao hii karimu hata kadiri gani bado haitoshi. Kwani, Waislamu hawajasahau zama zile walipokuwa wanateketea ndani ya tanuri liwakalo mikononi mwa taifa la Singasinga. Na kwa dhuluma zao si tu Waislamu waliharibiwa kidunia bali hali yao kidini ilikuwa mbaya zaidi. Achilia mbali kutekeleza faradhi za kidini, baadhi yao kwa kutoa tu adhana walikuwa

wanauawa. Katika hali hiyo mbaya Mwenyezi Mungu Alituma kwa ajili ya ukombozi wetu serikali hii yenye baraka kutoka mbali kama wingu la rehema, ambayo ikija si tu ikatukomboa katika makucha ya wadhalimu hao, bali kwa kuweka amani ikatoa vitu vitupatiavyo raha vya aina zote, na ikatupatia uhuru wa kidini kiasi hiki kwamba twaweza kueneza dini yetu thabiti bila hofu yoyote kwa njia bora. Kwenye Idul Fitri tulitoa hotuba kwa kirefu juu ya mada hii ambayo muhutasari wake umeshatumwa kwa magazeti ya Kiingereza, na taarifa kwa utondoti si siku nyingi ataichapisha mpendwa wangu kwa ajili ya Mungu, Mirza Khuda Bakhsh. Sisi, wakati wa Idi hii yenye baraka kwa kutaja hisani za serikali tulielekeza Jumuiya yetu yenye ikhlasi ya dhati kwa serikali hii na ambayo inaona kuishi kinafiki kama watu wengine kuwa dhambi kubwa kwamba watu wote waombe kwa moyo mkunjufu kwa serikali yao hii yenye hisani kuwa Mwenyezi Mungu Aijalie ushindi adhimu katika vita hii inayoendelea kule Transvaal. Na nilisema hii pia kwamba baada ya haki za Allah, faradhi kuu ya Islam ni kuwahurumia mahuluku, na hususani kuwahurumia watumishi wa serikali yenye hisani kama hiyo, ni jambo la thawabu, inayolinda uhai wetu na mali zetu, na zaidi ya yote dini yetu. Hivyo, wanajumuiya wetu popote walipo watoe mchango sawa na uwezo na wasaa wao kwa ajili ya majeruhi wa serikali

ya Kiingereza waliojeruhiwa katika vita ya Transvaal. Basi, kwa tangazo hili wanajumuiya wetu wanapashwa habari kwamba kwa kukamilisha orodha katika kila mji na kwa kukusanya mchango, watume Qadian kwa Bwana Mirza Khuda Bakhsh kabla ya Machi mosi, kwani yeye ndiye aliyekabidhiwa jukumu hili. Zitakapofika fedha zenu pamwe na orodha, ndipo orodha hiyo ya mchango itatiliwa katika taarifa iliyotajwa hapo juu. Jumuiya yetu itekeleze haraka sana kazi hii kwa kuifahamu ni ya lazima sana.

Wasalam.

Mwandishi: Mirza Ghulam Ahmad kutoka Qadian, 10 Februari 1900.

Habari Njema

Katika tangazo la Februari 10, ulidhihirishwa utashi kuwa pamwe na taarifa, orodha ya majina ya watoa mchango itachapishwa, lakini kwa kuwa taarifa imekuwa ndefu, hivyo Hadhrat Imam Mtukufu, Mwongozi wa mahuluku anaonelea kwamba orodha isichapishwe. Kiasi kikubwa kikubwa kimepokelewa kutoka kwa watu wachache tu wengine wametoa kiasi kidogo kidogo sana. Mchango mkubwa zaidi ni rupia 150 aliotoa

Nawab Muhammad Ali Khan, chifu wa Malerkotla na mchango wa chini kabisa ni *pai* [8] tatu.

Kwa kuwa Hadhrat Mtukufu Janabi Masihi Mau'udi[as] hapendi kukawia zaidi kutuma fedha, kwa hiyo baada ya kusubiri hadi tarehe iliyowekwa katika tangazo, kiasi cha rupia 500 kilitumwa kwa mheshmiwa Katibu Mkuu wa Serikali ya Panjab, na stakabadhi tuliyopokea kutoka kwa mheshimiwa huyu tunainukuu mbele. Lakini, kabla hatujainukuu risiti, tungependa kubainisha kwamba Hadhrat Mtukufu[as] amewafurahia sana waliowahurumia na kuwasaidia majeruhi, wajane, na mayatima wa serikali ya Kiingereza sawa na uwezo na wasaa wao. Na ni pongezi kwa wale ambao kwa kutekeleza agizo la Imamu wa kweli, si tu wamemfurahisha mwongozi wao bali wamekuwa sababu ya kupata ridhaa ya Mmiliki wa kweli wa ufalme na furaha ya watawala wa kimajazi. Kwani, Mfalme wa mbingu na ardhi Ameagiza vikali ndani ya Kitabu Kitukufu kilichopo mkononi mwa Waislamu kuzingatia haki za mahuluku baada ya haki za Allah, na Ameitaja kuwahurumia binadamu kuwa sababu ya furaha na ridhaa Yake. Bila kujali mtu kuwa wa dini au taifa gani, akiwa ni wa mashariki au wa magharibi, Ameagiza kuwahurumia wote. Tena, yule aliye mhisani na anayelinda haki zetu, kumhurumia ni

[8] *Pai* ni sarafu ndogo ya shaba, thamani yake ni sawa na theluthi ya pesa.

jukumu letu la kwanza kabisa. Ni nani aliye mhisani na mtakia heri zaidi kuliko Serikali hii ya Kiingereza ambayo mahali pengi imewasaidia Waislamu, na kwa kuwakomboa katika masaibu yenye hatari na mateso imewapa kimbilio kwenye hifadhi ya amani na usalama.

Mchango uliotumwa na Jumuiya hii yenye hali ndogo, ulikuwa haba sana kulingana na serikali hii yenye shani kubwa, lakini serikali hii yenye moyo mkubwa ilipokea kwa heshima kubwa na pia ilionyesha furaha yake. Ni wenye bahati njema watu ambao wakishiriki katika furaha na huzuni ya watawala wa wakati wanazingatia hadhi ya kutawala na kutawaliwa. Yenye maadili na shani kubwa iliyoje Serikali inayoheshimu na kuthamini michango haba na pongezi za raia wake. Je ni jambo dogo hili la kuheshimu kwamba Janabi Mheshamu Nawab Luteni Gavana, akatuma risiti ya kufurahia kiasi kidogo cha rupia 500 tu. Na kwa kumtumia barua ya pongezi juu ya kupata ushindi huko Afrika kusini, Mheshmiwa Nawab Gavana Mkuu, Kaimu Mfalme, na Mheshmiwa Gavana wa Panjab, kila mmoja wao, katika barua zao wameonesha furaha na kumshukuru Hadhrat Masihi Mau‘udi mwongozi wa mahuluku. Alakullihali, Serikali hii inastahiki kushukuriwa. Mwenyezi Mungu Aidumishe muda mrefu serikali hii inayohami amani na uhuru, na Aijaalie sehemu kubwa katika ufalme wa mbinguni.

Sasa, hapa chini tunaandika tafsiri ya barua zote tatu ili wasomaji waburudike kwa kuzisoma.

Barua Na. 234

Kutoka kwa J.M.C. Dowie, I.C.S. Kaimu Katibu Mkuu wa Serikali ya Panjab.

Kwa Bwana Mirza Ghulam Ahmad chifu wa Qadian, wilaya ya Gurdasapur, mnamo 26 Machi 1900 kutoka Lahore.

Mpendwa Bwana! tumeagizwa na Nawab Luteni Gavana kukuarifu kuwa mchango wa ukarimu wa rupia 500 uliotumwa kutoka kwako na wafuasi wako kwa ajili ya wagonjwa na majeruhi wa Afrika kusini wa serikali ya Kiingereza, umepokelewa na umekwishatumwa kwa King Kong Kampuni huko Bombay.

Mwandishi

Mtiifu wako

J.M.Dowie, Kaimu Katibu Mkuu wa Serikali ya Panjab

Barua Na. 166

Tarehe 9 Machi 1900 kutoka Lahore

Kutoka W.R.H. Merk C.S.I., Kaimu Katibu Mkuu wa Serikali ya Panjab.

Kwa Bwana Mirza Ghulam Ahmad Chifu wa Qadian, wilaya ya Ghurdaspur.

Mpendwa Bwana! nimeagizwa na Mheshmiwa Nawab Luteni Gavana nikuarifu kwamba yeye anakushukuru kwa furaha kubwa kutokana na pongezi uliyotoa kuhusu ushindi, ilioupata Serikali ya Kiingereza huko Afrika kusini.

Mtumishi wako mtiifu sana

W. Merk, Kaimu Katibu Mkuu wa Serikali ya Panjab.

Barua Na. 211

Kutoka kwa W.R.H. Merk C.S.I., Kaimu Katibu Mkuu wa Serikali ya Panjab

Kwa Bwana Mirza Ghulam Ahmad Chifu wa Qadian, mnamo 21 March 1900 kutoka Lahore

Mpendwa Bwana! nimeagizwa nikujulishe kwamba Serikali ya India imepokea kwa furaha sana pongezi uliyotoa kwa Serikali ya Kiingereza juu ya ushindi ilioupata Serikali kule Afrika kusini.

Mtumishi wako mtiifu sana

W. Merk, Kaimu Katibu Mkuu wa Serikali ya Panjab.

Tafsiri ya barua ya Kiingereza

Na. 307, 18 April 1900

Stakabadhi yenyewe ipelekwe kwa Bwana Mirza Ghulam Ahmad, mkazi wa Qadian wilaya ya

Ghurdaspur, ikiwa ni Barua Na. 234 ya ofisi hii ya tarehe 26 Machi 1900.

Kwa agizo la Katibu Msaidizi wa Serikali ya Panjab, Sahihi ya Katibu Msaidizi

Tafsiri ya stakabadhi ilivyo ya Kiingereza D Na. 1438, Mfuko wa Mstahiki Meya

Huu ulianzishwa kwa kuwasaidia wajane, mayatima na majeruhi wa Transvaal. Kiasi cha rupia 500 kilipokelewa kutoka Bombay mnamo 31 March 1900 kutoka kwa Bwana Mirza Ghulam Ahmad, mkazi wa Qadian, wilaya ya Gurdaspur, na wafuasi wake. Mchango huu ni kwa ajili ya Mfuko uliotajwa hapo juu, kwa njia ifaayo itumwe kwa Mheshmiwa Sana Mstahiki Meya.

Sahihi ya keshia, King Kong Kapmuni

Imehaririwa na Mirza Khuda Bakhsh kutoka Qadian.

Kasida ya Bwana Maulawii Abdullah Mkashmiri

Sifa zote njema ni kwa Mlezi Wetu Ambaye uzuri wa uso Wake umedhihirika katika kila dhihirisho Lake.

Aliyetia kivuli cha sifa zake kwenye madhihirisho Yake, ili uwepo wetu ukamilike katika dunia.

Kwa ajili ya mwili wetu, uwepo wetu, na kuendeleza maisha yetu Ametujalia mahitaji yetu yote yasiyohesabika.

Kila kitu cha lazima kwa mwili na uhai wetu Ametuandalia hicho Muumba Mwenyewe kwa rehema Yake.

Jua na mwezi, nyota, ardhi hii na mbingu, maakuli na mavazi, na matunda matamu,

Upepo huu mwananana unaovuma muda wote kwa ukarimu Wake, bustani hizi na *maua ya* tulipu na maporomoko ya maji,

Hivi vyote ni rehema na hisani za Dhati Adhimu, pasipo fadhili zake zama hizi zitakuwa zenye giza totoro.

Kila aina ya hamdu inampasa Yule Dhati wa kweli Ambaye uzuri wa hisani Zake ni bahari isiyo na kikomo.

Kutokana na fadhili na wema Wake, hekima na shani Yake kuu, rehema Yake ikadhihirika vizuri mno duniani kupitia madhihirisho Yake.

Kwa sababu ya ulezi Wake Ameonesha uso Wake kupitia dhihirisho Lake, ili Awe Mwenye kutuneemesha mwili wetu na roho yetu.

Na uwepo wa wazazi pia ni kivuli cha Mola wa watu; ndiyo maana mama anampakata mtoto wake.

Sikilizeni nukta moja kukamilisha khulka ya kibinadamu, tazameni vizuri madhihirisho na Mkumbukeni Muumba.

Kuwashukuru walio madhihirisho ya hisani za Mungu ni kumshukuru Yeye, na kwa imani yenu kumbukeni daima: 'Asiyewashukuru watu, hamshukuru Mungu'.

Mungu Mkweli Alisema, Enyi waaminio, fanyeni hisani kwa wazazi wenu, na uhakika wa siri hii ya hisani Yake imedhihirika kwa ulimwengu.

Mwongozi kwenye dini na tauhidi ya Mungu wa milele, akawa dhihirisho la Mwumba wetu kwa ajili ya roho yetu.

Zama hizi zimechomoza Jua hili juu ya dunia kutoka India, kama jua la kichwani.

Nawezaje kumtukuza ipasavyo mfalme huyu mwenye shani kubwa; nawezaje kujua sifa za uso wa mtukufu huyu.

Seyidna, Mwongozi wetu, na Mkuu wa dini yetu, ni ashiki wa uso wa Muhammad[saw] saa zote kwa harara ya shauku kubwa.

Uso wake Mtukufu unatoa mnukio wa Mpendwa wa azali, na shungi zake zatoa harufu nzuri ya miski.

Amemulika duniani kama jua linaloangaza ulimwengu, na maji yametiririka vijitoni, yaletayo uzima kwa imani.

Kwa hewa safi ya nuru ya imani bustani ya moyo imepata marini, na upepo wa Rabiu (majira ya kuchipua) unavuma kwa watu wenye tabia njema.

Kurumbiza ametoa vilio bustanini mwa Muhammad[saw], na kuifanya bustani iliyoharibiwa kustawi.

Huyu mwenye tabia iliyobarikiwa ni kurumbiza katika bustani ya utakaso; kwa vilio vyake macho ya mioyo ya wakweli yakatiririsha machozi.

Katika daraja ya ukaribu na Mwenyezi Mungu amekanyaga kileleni, na kwa mvinyo ya mapenzi ya Mohammad[saw] amejisahau dhati yake.

Mwenyezi Mungu kwa neema zake Amemtukuza duniani, na akapata heshima Barazani mwa Mjuzi, Mwenye nguvu.

Akashuka kutoka mbinguni hapa Qadian. Katika zama hizi mvua ya rabiu imenyesha juu ya ardhi iliyokufa.

Kwa ajili ya kumsadikisha sauti ikatoka mbinguni, vile vile jua na mwezi, mwezi wa Ramadhani na kimondo *vikahakikisha ukweli wake*.

Isa mwenye sera njema na Mahdi wa zama za mwisho amekuja kwa kukanusha wazo la kupigana.

Kwa ajili ya kuwafanya wapiganaji hao washindwe, ambao kwa mwenendo wao Islam imefedheheka sana,

Huyu Imamu wa zama amefika ili adhihirishe, kwa ukweli na unyofu, siri ya imani duniani.

Ndani ya Kurani ya Mungu Karima, Amesema 'Mfalme wa watu', na hiyo ni ishara wadhiha kwenye mfalme huyu,

Kwa ajili ya mahuluku, mfalme mwadilifu amekuwa kivuli cha Mungu duniani kwa hisani ya Mungu.

Kila asiyemshukuru mfalme mwadilifu, anafedheheka na kudhalilika pia mkadhibishaji kama huyo wa neema za Mwenyezi Mungu.

Nabii yule mtukufu na mfalme wa Manabii[saw], aliipatia enzi ya Kisra heshima na fahari.

Ni amri ya Huyo Mtukufu, watendee kwa wema walio wema, na wakunjie uso waovu wenye kijicho.

Ni faradhi kwa mahuluku wa Mungu kutambua haki, na wasiotoa shukrani kwa neema za Mungu watakuwa na makao mabaya.

Ilimuradi, katika zama njema za mfalme huyu wa India, kwa hisani yake majira ya kupukutika kwa majani yakawa majira ya kuchipua.

Kivuli cha uadilifu wa dola hili kimeenea kila upande. Katika zama hizi hizi ameshuka duniani Mahdi Mtukufu mwenye kufuzu.

Serikali hii ni kivuli cha Mwenyezi Mungu juu yetu; na zama za wadhalimu waovu nazo pia zapaswa zikumbukwe.

Aliyeshuhudia zama za Singasinga, anakumbuka dhuluma; wao walifanya uonevu na ukatili mwingi.

Walikuwa wanazua maafa kwa adhana kutolewa; na kwa ajili ya ng'ombe mmoja watu walikuwa wanachomwa motoni.

Kutokana na dhuluma zao dunia ilikuwa kama usiku wenye giza nene; ghafla akatokea mfalme mwenye mwanga.

Serikali hii njema ilipotanda kivuli chake juu yetu, mara usiku wetu, kwa rehema ya Mungu Mwenye enzi, ukabadilika kuwa mchana.

Kwa uwepo wa dola hili amani na utajiri ukapatikana, na kwa kuimarisha imani mpanda farasi bingwa akashuka kutoka juu.

Ili kukamilisha hoja, Mungu Wake Akamteremshia kutoka mbinguni hazina ya maarifa na upanga mkali.

Kwa mkuki wa kimbingu akamuua dajali chongo, na makazi ya Atham mwenye jicho moja pia yakawa Jahanamu.

Lekhramu msimbo pia akauawa kwa upanga mkali, na Waariya wenye tabia mbaya pia wakafedheheshwa siku hiyo na Mungu.

Mfu Ishvar [mungu wa Mabaniani] asiye na nguvu, hakuwa na uwezo wa kumsaidia wakili mwenye mdomo mchafu.

Kijana huyu [Seyidna Ahmad[as]] kwa hakika ni tawi la mti wa bustani ya Peponi. Mlimaji wa bustani Akalimwagilia, nalo likawa mti wenye kuzaa matunda.

Kila apigaye shina lake kwa msumeno kwa ujinga, kwa hakika anajikata miguu yake, na roho yake inateketea pia motoni.

Pajini pake nuru ya haki inang'aa daima kwa unyofu, na mnukio wa nywele zake nyeusi umesambaa duniani kama uturi.

Moyoni mwangu husisimka sifa ya mwezi mpevu huu uondoao kiza, lakini maelezo ya bahari isiyo na kikomo hushindikana.

Huyu ni mtumishi wa Mfalme wa wazuri aitwaye jina Mustafa[saw] – ndiye yule ambaye kwa tauhidi ya Mungu akayapiga masanamu shoka, yaliyokuwepo mlangoni pa nyumbaye.

Akaithibitishia dunia unyonge wa masanamu ya Manasara, na maiti mmoja wa zamani akajidhihirisha uso wake katika mtaa wa Khanyar [Kashmir].

Kurumbiza mwenye sauti tamu kutoka bustani ya Mtukufu, Jalali, akatua kwenye tawi la juu, anaimba nyimbo za mapenzi ya Mungu.

Mpigaji mwereka wa kimbingu mwenye heshima na shani kuu na ambaye malaika wapo kulia na kushoto kwake kumhudumia,

Ameonesha, kwa kudura ya Mungu mambo makuu ya nguvu ya haki, na amechana mapazia ya wakana, wala nyamafu.

Hakuna anayejitokeza uwanjani kukabiliana naye, na maadui wamejificha pembeni mwa pango wakibweka.

Ulimwengu ulitetemeka vikali alipotoa huyu [mwereka] mashuhuri wito uwanjani mwa vita.

Yu mwenyekiti mkutanoni, kiongozi na mwongozi wa waaminio. Ishara zafululiza kuipa nguvu dini.

Mji wa amani [Qadian] umepambwa na baraka za kimbingu; pia mahuluku na ulimwengu na sehemu za jirani zimemulika.

Kwa ukweli na usafi wa moyo yeye amekuwa mwenye kuitakia heri serikali, si kwa hila na kuivika kilemba cha ukoka, bali kwa amri ya Mwumba.

Mungu Ameshasema, wafanyie wema wafanyao wema, basi jahili na mpumbavu anakataa jambo hili.

Jahili akikaa msikitini anatulaumu, kwa sababu ya sisi kumtakia heri mfalme mwenye heshima.

Hatuogopi hao wenye tabia ya mbwa kubweka, bali tunaona haya na aibu kuwa na unafiki, na khulka mbaya.

Tunamwomba Mungu bahati njema kwa mfalme wa India; tuna uhusiano gani na hawa wapenda dunia, wenye tabia chafu.

Ee Mwabudiwa wa watu, daima tunapaswa kujikinga kwako katika madhara ya adui wa kudumu ambaye huuma kama nyoka.

Ee Mungu wa nchi na ulimwengu, na kimbilio la wakweli, Uifanye mvua ya rehema iinyeshee ardhi ya wakweli.

Watu wabaya wanaoipa migongo haki, moto utaanguka vichwani pao utakaong'olea mbali mizizi ya wachafu.

Nitupie jicho mahangaiko yangu na nijalie neema zako, na nileweshe kwa mvinyo ya upendo wa Imamu wa ulimwengu.

Masihi wa Qadian ampendaye sana sana Mbora[saw] wa mahuluku wote, rehema ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya roho yake duniani na Akhera.